KWAYA YA MTAKATIFU KIZITO
PAROKIA YA MWENYEHERI ANUARITE MAKUBURI
+255742000089|+255713975788
kmkmakuburi
www.kmkmakuburi.co.tz
stkizitochoir@gmail.com

SIMBA WA YUDA-J. SALISALI

Kiitikio

(Hee! Hee! Hee! Amefufuka) x2 Yesu ni mzima simba wa Yuda kashinda vita, Nguvu za kuzimu kimya kazinyamazisha,(tumshangilie na twimbe aleluya, Makofi tupige na na vigelegele, Ameshinda mauti Bwana amefufuka) x2

Mashairi

1. Maajabu ya Mungu tumeyaona,(He) Yasiyowezekana ameyafanya,(He) Kadhihirisha, ukuu wake, Ndiye Mungu, Awe-e-zaye,
   Kwa maringo ngoma madaha ya kikwetu vinywa vyetu viimbe na viseme…

2. Siku tatu amekaa kaburini,(He) baadaye katoka ametakata (He),
   Yesu mshindi vita kashinda, anastahili heshima zote, Kwa maringo…

3. Safari ndefu kwake Bwana ni fupi(He),giza nene kwa Yesu sio chochote (He) ona kang'ara anamulika, kwa kufufuka twaona njia,Kwa maringo…..

4. Ni zawadi ya uzima ametupa (He), kafufuka mwokozi katuhuisha (He), tumefufuka pamoja naye, milele yote hatufi tena, Kwa maringo…..

Hitimisho

Mbinguni shangwe washangilia, (Bwana) Ameshinda mauti Bwana amefufuka. Dunia yote yanshangilia, (Bwana) Ameshinda mauti Bwana amefufuka. Vurugu za dunia zimetulizwa zimenyamaza (Bwana) Ameshinda mauti Bwana amefufuka. Tunaimba tunacheza, tumefurahi, Ameshinda mauti Bwana amefufuka. Tunaimba tunacheza, tumefurahi, Ameshinda mauti Bwana amefufuka